**MAELEKEZO YA MHESHIMIWA CHARLES MAKONGORO NYERERE MKUU WA MKOA ALIYOYATOA KWENYE KIKAO CHA BARAZA LA MADIWANI HALMASHAURI YA MANISPAA YA SUMBAWANGA KUHUSU UTEKELEZAJI WA HOJA ZA UKAGUZI NA MAPENDEKEZO YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI KWA MWAKA 2021/2022 KILICHOFANYIKA KATIKA UKUMBI WA HALMASHAURI TAREHE 13 JUNI, 2023.**

- ***Mstahiki Meya wa Manispaa,***
- ***Katibu Tawala Mkoa,***
- ***Ndg. Mwenyekiti wa CCM wa Wilaya Sumbawanga Mjini,***
- ***Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya ya Sumbawanga,***
- ***Waheshimiwa Madiwani,***
- ***Mkaguzi Mkuu wa Nje wa Mkoa kutoka Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali,***
- ***Wataalam kutoka Sekretarieti ya Mkoa,***
- ***Katibu Tawala wa Wilaya ya Sumbawanga,***
- ***Wataalamu wa Halmashauri ya Manispaa,***
- ***Wageni Waalikwa,***
- ***Waandishi wa Habari,***
- ***Mabibi na Mabwana.***

**Nawasalimu kwa jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania…………..**

***Mstahiki Meya wa Manispaa,*** Awali ya yote napenda nitumie nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutujalia sisi sote kuwa na afya njema. Kwa namna ya pekee nimshukuru na kumpongeza **Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan**, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu kwa namna anavyoiongoza nchi yetu kwa weledi mkubwa na kuitangaza nchi yetu Kimataifa. Namshukuru **Mh. Dkt. Samia Suluhu Hassa**n kwa kuendelea kuniamini na kuniteua kuwa Mkuu

wa Mkoa wa Rukwa, Aidha nimshukuru sana kwa kutuletea fedha nyingi kwenye miradi mbalimbali ya maendeleo ya Wananchi kwenye Sekta za Afya, Elimu, Miundombinu ya Barabara, na Maji.

***Mstahiki Meya,*** Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga kwa Mwaka wa Fedha 2021/22 imepata Hati yenye Shaka. Sababu zilizopelekea kupata Hati yenye shaka ni mapungufu au udhaifu katika uandaaji wa hesabu na kupelekea kupata hoja sita (6) kama ifuatavyo;

- Mali za kudumu, mitambo na vifaa kuripotiwa chini ya thamani yake kwa shilingi 1,429,249,706 kwa kipindi cha kuishia Juni, 2022.
- Taarifa ya madeni (payables) kuripotiwa pungufu kwa shilingi 256,193,524
- Mali za kudumu, mitambo na vifaa kuripotiwa zaidi ya thamani yake kwa kipindi cha kuishia Juni, 2021 kiasi kilichozidi ni shilingi 270,000,000
- Ongezeko la salio anzia (Opening balance) katika taarifa ya malimbikizo ya ziada (Accumulated surplus) kiasi cha shilingi 403,746,000
- Ongezeko la gharama za ununuzi wa vifaa vya Ofisi katika taarifa ya mtiririko wa fedha (cash flow statement) kwa shilingi 348,194,796.
- Gharama za ununuzi wa mali za kudumu kuoneshwa pungufu katika taarifa ya mtiririko wa fedha kwa kiasi cha shilingi 3,206,694,181.

Ni dhahiri kuwa hakukuwa na umakini wa timu iliyohusika na uandaaji wa Hesabu, vile vile taarifa zilizotolewa na idara mbalimbali za Halmashauri kwa ajili ya uandaaji wa Hesabu hazikuwa sahihi au hazikujitosheleza.

***Mstahiki Meya,*** Mwenendo wa ukusanyaji wa mapato katika Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga kwa miaka mitatu

mfululizo mmekusanya zaidi ya asilimia 100 ni jambo zuri na napenda kuwapongeza kwa hili. Pamoja na ukusanyaji huo bado napenda kutoa wito kuhakikisha mnafanya makisio yenye uhalisia kwa kuongeza makisio kwa bajeti zijazo kwani pamoja na kiasi hicho kukusanywa kwa asilimia 100 bado Halmashauri inakabiliwa na changamoto nyingi za uendeshaji wa Shughuli za Halmashauri ikiwemo madeni ya Watumishi na watoa huduma mbalimbali.

***Mstahiki Meya*****,** Katika Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mwaka 2021/2022 iliyotolewa Aprili, 2023 ilionyesha kwamba Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga ilikuwa na Hoja za miaka ya nyuma ambazo hazijafungwa **17** na Hoja za Mwaka huu (2021/2022) **21** hivyo kufanya Jumla ya Hoja **38**. Natambua Mkoa kupitia Vikao umesisitiza Halmashauri kujibu Hoja hizi ili ziweze kufungwa. Kupitia Kikao hiki nimtake Mkurugenzi na Wataalam wake kushirikiana na Mkaguzi wa Nje kuhakiki Hoja hizi zilizosalia ili ziweze kufungwa. Pamoja na Hoja hizi zipo Hoja ambazo ningependa kusisitiza hapa kama ifuatavyo: -

1. Taarifa ya CAG imeonyesha kwamba uwasilishaji wa Taarifa za Fedha zilikuwa na mapungufu (Submitted Financial Statements with Material Misstatements). Halmashauri inapaswa kuhakikisha inaandaa taarifa ya Hesabu za Mwisho kwa viwango vinavyokubalika ili kuepusha mapungufu hayo yasijitokeze tena katika Hesabu za Mwaka ujao ambao unakwenda kuisha tarehe 30 Juni, 2023. Nimtake Mkurugenzi kuchukua hatua stahiki kwa watumishi wote waliohusika na uandaaji na walishindwa kutoa taarifa sahihi kwa timu iliyohusika na uandaaji wa Hesabu.
2. Eneo lingine lenye Udhaifu ni Usimamizi wa Miradi ya Maendeleo. Katika taarifa ya CAG amebainisha Mapungufu mengi yakiwemo: -

- Kutokukamilika kwa baadhi ya shughuli katika Stendi ya Mabasi ya Katumba Azimio zenye thamani ya Sh. 728,454,193
- Kutokukamilika kwa Miradi ya Kituo cha Afya Mollo, Kituo cha Afya Matanga, Shule ya Sekondari Momoka, na Zahanati ya Mponda.

Nimtake Mkurugenzi ahakikishe miradi inasimamiwa kikamilifu ikiwemo kufuata taratibu na miongozo ya utekelezaji wa miradi hiyo ili kupunguza hoja zisizo na ulazima, kuhakikisha thamani ya fedha inaonekana kwani Serikali inaleta fedha nyingi ili Wananchi waweze kupata Huduma na kuchukua hatua stahiki kwa watumishi wote waliosababisha kutokamilika kwa miradi hiyo.

3. Eneo la Manunuzi**,** katika taarifa ya CAG, imeonekana Halmashauri ina Udhaifu katika uzingatiaji wa Sheria na Taratibu za Manunuzi za mwaka 2011 pamoja na Kanuni zake za mwaka 2013 pamoja na usimamizi wa Mikataba. Eneo hili ndilo lenye Hoja nyingi kuliko maeneo mengine na limekuwa na athari kubwa katika utekelezaji wa miradi, na kwa tathmini mapungufu mengi katika miradi yanatokana na eneo hili la manunuzi hivyo Halmashauri inapaswa kutilia mkazo kitengo cha manunuzi kuhakikisha kinatekeleza majukumu yake kwa kuzingatia Sheria, Taratibu na Kanuni za manunuzi ili kuepusha Hoja aidha utendaji wa Mkuu wa Kitengo cha manunuzi ufuatiliwe. Baadhi ya Hoja katika eneo la Manunuzi zilizobainishwa katika Taarifa CAG ni pamoja na: -
    - Nukuu za Bei (Price Quotations) zilizotolewa kwa wazabuni bila kuwa na maelezo ya bidhaa zinazonunuliwa Sh.218,811,381
    - Malipo kufanyika kabla ya kupokelewa kwa bidhaa Sh.234,576,950
    - Malipo yaliyofanyika kwa Bidhaa/Huduma ambazo hazikupokelewa Sh.327,646,230

- Manunuzi yaliyofanyika kwa wazabuni ambao hawalingani Sh.433,760,515
- Mapungufu katika nukuu za bei za manunuzi yenye thamani ya Sh. 333,876,774

4. Eneo la mapungufu katika upelekaji wa asilimia 40 ikiwemo asilimia 10 ya Mfuko wa Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu kutokana na Mapato halisi bila lindwa yanayokusanywa na Halmashauri. Pia Kutopelekwa kikamilifu kwa Asilimia 10 ya Mapato ya Ndani kwenye Mfuko wa Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu kiasi cha Shilingi 96,193,729. Mkurugenzi Wa Halmashauri hakikisha kuwa Asilimia 40 ya Maendeleo inapelekwa kama sheria inavyotaka.

***Mstahiki Meya,*** Pamoja na maelekezo niliyoyatoa wakati wa uchambuzi wa hoja za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali naomba nitoe maelekezo ya jumla kwa Halmashauri yako ili kupunguza na kuepuka Hoja za Ukaguzi kama ifuatavyo: -

i. Nasisitiza hatua stahiki za kinidhamu na kiutumishi zichukuliwe kwa watumishi wote ambao wameonekana kusababisha hoja kutokana na uzembe bila kumuonea mtu kwa kufuata taratibu na sheria na taarifa iwasilishwe Ofisi ya Mkuu wa Mkoa kabla ya Tarehe 25 Juni, 2023.
ii. Halmashauri ihakikishe kuwa Uandaaji wa Taarifa za Fedha (Financial Statement) kwa kuzingatia Viwango vya Kimataifa vya Uandaaji wa Taarifa za Fedha katika Sekta ya Umma (IPSAS), Waraka wa Uandaaji wa Taarifa za Fedha wenye Kumb.Na:EG.03/102/09/18 wa tarehe 1 Juni, 2023 na kutenga muda wa kutosha kuhakiki taarifa hizo kabla ya kuwasilishwa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi.
iii. Kutoa ushirikiano kwa Wakaguzi wa Nje pindi wanapofanya Ukaguzi badala ya kusubiri Hoja za Ukaguzi na Wakuu wa Idara na Vitengo husika wakatoe maelezo au ufafanuzi kwa

wakaguzi badala ya kuwatumia Wasaidizi. Hii itasaidia baadhi ya Hoja kuisha wakati wa Ukaguzi unapoendelea.

iv. Halmashauri ihakikishe inaongeza wigo wa makisio ya mapato ya ndani kwa kuwa wabunifu wa kutafuta vyanzo vipya badala ya kutegemea vyanzo vile vile ambavyo haviongezi tija,

v. Halmashauri iimarishe usimamizi wa manunuzi kwa kuhakikisha Sheria na Taratibu za manunuzi zinafuatwa kikamilifu. Aidha kabla ya Manunuzi kufanyika katika miradi ya maendeleo kuwepo kwa mchanganuo wa gharama (schedule of requirements/materials) ili kutoruhusu ununuzi holela wa vifaa au zaidi ya mahitaji.

***Mstahiki Meya,*** Mwisho, Napenda kukushukuru tena wewe pamoja na Waheshimiwa Madiwani na timu ya Menejimenti ya Halmashauri kwa kunialika kuhudhuria kwenye kikao hiki muhimu. Asanteni sana.

Mungu Ibariki Tanzania,

Mungu Ibariki Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga

Asanteni kwa Kunisikiliza.

Charles Makongoro Nyerere

**MKUU WA MKOA RUKWA**